ASAS kuanza kuzalisha maziwa ya unga

Na Frank Leonard, Iringa

KAMPUNI ya maziwa ya Asas inatarajia kuwa ya kwanza nchini kuanza uzalishaji wa maziwa ya unga katika mpango wake unaolenga kuongeza bidhaa zitokanazo na maziwa na kuhamasisha jamii kutumia bidhaa hizo zinazozalishwa nchini.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki alipokea taarifa hiyo akisema itasaidia kuokoa fedha nyingi za kigeni zinazotumika kuagiza maziwa hayo nje ya nchi.

Alisema hayo juzi alipotembelea kiwanda cha kampuni hiyo mjini Iringa na shamba lao la mifugo Igingilanyi, nje ya mji wa Iringa kwa lengo la kujionea shughuli zao za uzalishaji na ufugaji.

"Kuna mahitaji makubwa sana ya maziwa ya unga nchini. Na ni kwa bahati mbaya kwa sasa hatuna kiwanda kinachozalisha maziwa hayo.

Kampuni ya Asas mtakuwa wa kwanza mara mtakapoanza uzalishaji wake," alisema.

Awali Mkurugenzi wa Kampuni ya Maziwa ya Asas, Fuad Abri alisema kampuni yao yenye uzoefu katika sekta hiyo ya maziwa kwa miaka 30 sasa itaendelea kubuni bidhaa mbalimbali za maziwa na kuingiza sokoni ili kukidhi mahitaji ya soko.

"Tulianza kwa kutembeza maziwa mitaani, changamoto ya soko ikatulazimisha kuanzisha kiwanda cha kusindika bidhaa mbalimbali za maziwa. Mwaka 2000 tulianza kusindika maziwa katika kiwanda chetu, tukiwa tumeanza na lita 1,000 kwa siku na sasa kiwango kimepanda hadi lita 44,000 kwa siku," alisema.

Pamoja na kupanda kwa uzalishaji huo, Abri alisema kiwanda chao kina uwezo wa kuzalisha lita 150,000 za maziwa.

Hata hivyo, alisema kinakwama kufikia mahitaji hayo kwa sababu ya uzalishaji mdogo wa maziwa kutoka kwa wafugaji. Soko kuu la bidhaa za maziwa ni Dar es Salaam huku wakiwa wamefika katika mikoa yote nchini.

Katika kuchochea shughuli za ufugaji na uzalishaji wa maziwa kwa kila ng'ombe, alisema kampuni yao yenye wafanyakazi 200 inafanya kazi na wafugaji wadogo 6,000 katika mikoa ya Iringa, Njombe na Mbeya, ina vikundi 139 vya wafugaji na ina vituo 13 vya kukusanyia maziwa.

Pamoja na juhudi zao za kuikuza sekta hiyo, Abri alishangazwa na kiwango cha unywaji wa maziwa nchini akisema si cha kuridhisha kwani takwimu zinaonesha mtu mmoja anakunywa wastani wa lita 55 kwa mwaka wakati Shirika la Afya Duniani linashauri atumie lita 200.

Scanned with CamScanner

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

Telegram:"Uvuvi"
Simu: 255 26 2322612
Nukushi: 255 26 2322613
Barua pepe: ps@uvuvi.go.tz
Tovuti:www.mifugouvuvi.go.tz

Mji wa Serikali Mtumba
Mtaa wa Ulinzi
S.L.P. 2847
40487 DODOMA

Dodoma
03 Januari, 2022

TAARIFA KWA UMMA

UTARATIBU MPYA WA USAFIRISHAJI WA BIDHAA ZA CHAKULA IKIWEMO MAZAO YA UVUVI NA MIFUGO KWENDA CHINA

Wizara inapenda kutaarifu umma kuwa serikali ya Jamhuri ya watu wa China kupitia mamlaka yake ya usimamizi wa forodha (General administration of customs of the people's Republic of china – GACC) imeweka utaratibu mpya wa kuingiza bidhaa za chakula katika nchi hiyo. (GACC order No. 248 & no 249) ambao utaanza kutumika kuanzia tarehe 01 Januari 2022

Hivyo Wizara ya mifugo na Uvuvi inapenda kuwatangazia Wafanyabiashara wanaosafirisha mazao ya chakula China kujisajili kwenye mamlaka ya forodha ya china kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi ambapo watapatiwa namba maalum za usajili zitakazotumika kwenye nyaraka za usafirishaji wakati wa usafirishaki aidha, wadau mnashauriwa kutembelea tovuti ya mamlaka ya GACC http/cifer singlewlow cn kwa raarifa na maelekezo kuhusu matakwa ya soko la China

Mawasiliano zaidi kwa ajili ya utaratibu wa usajili yafanyike kwa Bw, Stephen Lukanga Mkurugenzi msaidizi kitengo cha uthibiti Ubora Masoko na mazao ya uvuvi kwa namba ya simu **0754 437234** au baruapepe stehenlukanga@uvuvi.go.tz na kwa Bw Melkizedeck Koddy Afisa uvuvi kwa namba ya simu **0754 209535** au barua **pepe melkizedeck.koddy@uvuvi.go.tz**

Imetolewa na

KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI
WIZARA YA MIFUNGO NA UVUVI

Scanned with CamScanner

Wafugaji watakiwa kufuga kibiashara

Na Mirandishi Wetu, IRINGA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amewataka wafugaji nchini kufuga kibiashara na kuachana na ufugaji wa kuchunga ambao tija yake imekuwa ndogo kwao na kwa taifa pia.

Ndaki alitoa rai hiyo jana alipotembelea shamba la kisasa la mifugo la Shaffer, mkoani hapa.

Akiwa katika shamba hilo akikagua shughuli mbalimbali zinazoendelea kwenye eneo hilo, alisema wanawashauri wafugaji kuanza kufuga kisasa na kuachana na ufugaji wa kiasili ambao sasa umeanza kupitwa na wakati.

"Tumekuwa hatuoni faida kwa mifugo yetu kwa sababu ya kung'ang'ania ufugaji wa kiasili, wafugaji tuanze kufuga kibiashara ili tuongeze tija ya mifugo yetu," alisema Ndaki. Aliongeza kuwa ili waanze kuona tija ya ufugaji wao ni lazima wabadilike na waache ufugaji wa kuzunguka kutafuta maeneo ya malisho na badala yake wawe na maeneo yao ya kufugia ambayo yatakuwa rahisi kufikiwa na wataalamu kwa ajili ya kuwapatia huduma zinazohitajika kwa mifugo yao.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, Bashiru Muhoja, alisema mwekezaji wa shamba la mifugo la Shaffer anauhitaji mkubwa wa chakula cha mifugo kama vile soya na mahindi.

"Mheshimiwa waziri, huyu mfugaji ana uhitaji mkubwa wa soya, mahindi na alfaalfa ambapo kwa sasa vyote anavitoa nchini Zambia. Hii ni fursa kwa wananchi wetu na tumeshaanza kuchukua jitihada na tuna orodha ya wakulima ambao wako tayari kulima mazao hayo kwa ajili ya kumuuzia mfugaji huyu," alisema Muhoja.

Msimamizi wa Shamba la Shaffer, Mahboob Malick, alisema wanashukuru serikali kwa ushirikiano mkubwa inaowapatia na kwamba wako tayari kuendelea kushirikiana nayo kwa lengo la kuboresha ufugaji nchini.

"Sisi tuko tayari kupokea vijana ambao wanataka kuifunza ufugaji. Wale hapa tutawafundisha namna bora ya ufugaji wa kisasa ili wawezeta ujuzi huu waende kuwafundisha na wenzao na hatimaye kuboresha ufugaji wetu," alisema Malick.

Scanned with CamScanner